
# LITUKUZENI JINA LA MUNGU

By Fr.G.G.Kayetta

*(Sifa na Shukrani)*






1. Jina lake Bwana, litukuzwe sasa hata milele,
   Viumbe vya Bwana, msifuni Bwana Mungu wenu.
   Toka maawio hata machweo ya jua,
   Sifuni jina lake (Bwana Mungu wenu), Msifuni Bwana Mwenyezi.

2. Enyi watumishi, msifuni Bwana kutoka mbinguni,
   mbingu nanyi maji, lisifuni jina la Bwana.
   Wafalme wa dunia nanyi watu wote,
   Wakuu nanyi wakazi (wote wa dunia), Msifuni Bwana Mwenyezi.

3. Enyi Malaika, msifuni Bwana kutoka mbinguni,
   Jua mwezi nyota, msifuni Bwana wa mabwana.
   Majeshi yake yote na yamsifu Bwana,
   Yeye ndiye Mtawala (wa mabwana wote), Msifuni Bwana Mwenyezi.